Ecolebooks.com

# SHINYALU SOUTH CLUSTER

## KISWAHILI DARASA LA 5 MUHULA WA TATU 2019

Mlango_1_ mwalimu_2_kiswahili_3_aliyekuwa wa _4_ kuingia katika darasa _5_la tano.kipindi_6_asubui kilikuwa_7_Alitusabai kama_8_desturi_9_.baada ya shughuli za hapa na pale darasa_10_, alianza kutueleza_11_kuandika hati safi_12_darasani_13_pia maishani_14_.kisha alituita_15_ubaoni tukaandika neno hati.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ulipofugwa | B. ulifunguliwa | C. ulipofunguliwa | D.ulipofungulia |
| 2. | A. ya | B. kwa | C. cha | D. wa |
| 3. | A. ndio | B. ndivyo | C. ndiye | D. ndiyo |
| 4. | A. kuanza | B. kuwanza | C. kwaza | D. kwanza |
| 5. | A.letu | B. yetu | C. mwetu | D. kwetu |
| 6. | A.ile ya | B. kile cha | C. hiyo ya | D.hiiya |
| 7. | A.yake | B. lake | C. wake | D.chake |
| 8. | A. iliyokuwa | B. lilivyokuwa | C. ilikuwa | D.ilivyokuwa |
| 9. | A. yetu | B.kwake | C. yake | D. wetu |
| 10. | A.ule | B. lile | C. zile | D. ni |
| 11. | A.jinsi ya | B.hali ya | C. vile ya | D. niniya |
| 12. | A.siku tu | B. siyo tu | C.sio tu | D. siye tu |
| 13. | A.mbali | B.pale | C.bali | D.vile |
| 14. | A.yetu | B.mwetu | C. zetu | D. wetu |
| 15. | A. moja | B. mmoja | C. mojawapo | D. mmoja mmoja |

**Jibu maswali 16-30 kulingana na maagizo**

16. Rafiki yako akikwambia "kwaheri" utajibu
    A. sawa B. ya kuonana
    C. alamsiki D. buriani
17. Ni neno lipi kati ya haya halipatikani katika ngeli ya A-WA _________
    A. paka
    B. kiziwi
    C. kuku
    D. mvua

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

18. Tegua kitendawili kifuatacho:
    nameza lakini sishibi ____________
    A. uji B. njema
    C. chai D. damu
19. Ni kikembe kipi hakikuambatanishwa sawasawa na kiumbe chake.
    A. Kifaranga – kuku
    B. Jana – nyuki
    C. Buu – chura
    D. Kimatu - nzige
20. Kamilisha methali hii
    ______ furaha ya kunguru
    A. Vita ya panzi
    B. Vita za panzi

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

C. Vita vya panzi
D. Mvita wa panzi

21. Mmea unaozaa ndizi huitwa
A. Mchai
B. Mgomba
C. Mbuni
D. mpunga

22. Robo tatu huandikwa ____
A. $^{3}/_{6}$
B. $^{1}/_{4}$
C. $^{3}/_{4}$
D. $^{3}/_{8}$

23. Tumia kiulizi kinachofaa
Kiti _______ kitanunuliwa
A. ngapi B. yupi C. lipi D. kipi

24. Chagua tarakimu sahihi
mia saba sitini na tisa
A. 796
B. 766
C. 769
D. 799

25. Kamilisha kitendawili
Achora lakini hajui akichoracho
A. Siafu
B. Konokono
C. Kalamu
D. chungu


26. Andika wingi
maji ya ziwa ni machafu
A. maji wa ziwa ni machafu
B. maji ya maziwa ni machafu
C. maji ya maziwa ni chafu
D. maji ya ziwa ni chafu

27. Sentensi ipi iliyo na matumizi sahihi ya –enye na -enyewe
A. kitabu chenye ninasoma kina picha chenyewe
B. mtoto mwenye afya anatembea mwenyewe
C. maneno yenye ulisema yenyewe nimeyasikia
D. kwenye uunasomea ni mbali

28. Udogo wa kichwa ni ______
A. kijikichwa
B. kakichwa
C. kijichwa
D. kijijichwa

29. Mlio mkali wa kufahamishi hali ya hatari kama vile wa gari la wagonjwa au la polisi huitwa ______
A. kuwika
B. kubweka
C. king'ora
D. kamsa

30. Hili ni umbo gani?



A. mraba B. duara
B. kopa D. mstatili

**soma ufahamu huu, kasha ujibu maswali**

Nyanya yetu ni mzee sana. Kwa kweli hawezi kufahamu mwaka aliozaliwa.lakini ukimwangalia usoni, utajua mara moja kuwa ana zaidi ya miaka mia moja. Meno yake yote yalihama nywele zake zimeng'oka na kichwa chake ni kama janga la sahara.

Kila jioni yeye huwasha moto nje ya nyumba yetu. Nasi wajukuu wake huenda kuota moto pamoja na kupata uhondo wa hadithi zake za kuvutia . zimejaa mafunzo mengi kuhusu heshima, madhara ya uchoyo, wivu, woga, kuwa jasiri na kufanya bidii kazini.

Nakumbuka jioni moja nyanya alituhadithia juu ya chui na kobe. Chui alikuwa na tabia ya kumchokoza kobe kila walipokutana kama wasemavyo wahenga kuwa mwenye nguvu mpishe, kobe alivumilia uchokozi wa chui. Siku moja, chui alimwezeka rafiki yake makofi mpaka akawa hawezi kuvumilia tena. Kobe akawaza na kuwazua jinsi atakanyolipiza kisasi. Mwisho akapata suluhisho.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Kobe alienda katika mzinga wa nyuki na kupata asali kidogo. Alimpelekea rafiki yake chui. Chui alipoionja asali hiyo alitaka aeleze inapopatikana ili aende kuchukua zaidi.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

“ Hutaamini hata nikikwambia,” kobe alitamka. Baada ya chui kumbembeleza kwa muda mrefu alimwambia kuwa asali hiiyo ni mavi ya nyani. Kusikia hayo, chui huyo ……..! aliondoka ili aweze kupata asali.

“ Mavi yangu hayatakupendeza hata kidogo,” nyani alimwambia chui. Alimpiga nyani kucha mpaka akanya. Alipoyaonja mavi hayo, alitambua kuwa si matamu kama asali aliyopewa na kobe. Alipandwa na hasira zaidi akaanza kumtafuta kobe. Alipandwa na hasira zaidi akaanza kumtafuta kobe. Ndiposa kobe huficha kichwa chake aonapo mtu akidhani ni chui. Wahenga walinena kobe akiinama anatunga sheria.

31. Umri wa nyanya yetu ni
    A. Miaka mia moja
    B. Chini ya miaka mia moja
    C. Zaidi ya miaka mia moja
    D. hatujaambiwa
32. Neno yake yote yamehama ina maana kuwa nyanya yangu ni
    A. kibyongo
    B. kiwete
    C. bubu
    D. kibogoyo
33. Lengo kuu la kuwa karibu na nyanya kila jioni ni______
    A. kufurahia chakula cha jioni
    B. kuota moto
    C. kupata hadithi zenye mafunzo
    D. kuwashia nyanya moto
34. Neno jingine lenye maana sawa na hadithi ni __________
    A. ngano B. mafumbo
    C. vitendawili D. methali
35. Kulingana na kisa hiki, ni nani aliyekuwa mchokozi
    A. kobe
    B. nyani
    C. chui
    D. nyuki
36. Mwisho, kobe alipata suluhisho la.
    A. Kulipiza kisasi
    B. Kupata asali
    C. Kupiga chui makofi
    D. Kuvumilia uchokozi
37. “ Hutaamini hata nikikwambia” ni nani aliambiwa maneno haya ______
    A. Kobe
    B. Chui
    C. Nyani
    D. nyanya
38. Nyuki hukaa mzingani kama vile mchwa hukaa ______
    A. kichuguuni
    B. kizimbani
    C. zizini
    D. kiotani
39. Kobe alilipiza kisasi kwa ____
    A. kumpiga chui makofi mazito maito
    B. kumdanganya nyani
    C. kumpatia chui asali
    D. kumdanganya chui
40. Hadithi hii inatufunza
    A. ni vizuri kuwachokoza
    B. tuwe tukilipiza kisasi
    C. tusiwadharau wanyonge
    D. tuwa tukiota moto kila jioni

**Soma kifungu kisha ujibu maswali 41-50**

Maji ni uhai. Maji huhitajika katika maisha yetu ya kila siku. Tunahitaji maji ya kunywa, kupika , kuoshea na kupatia mifugo yetu

Maji ni muhimu katika kilimo. Mimea haiwezi kustawi bila maji. Maeneo ya nchi ambayo hayana mvua au mito hayavutii watu wengi kuishi humo. Wenyeji wa sehemu hizo

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

hukabiliwa na ukame miaka nenda miaka rudi. Baadhi yao hufa kwa njaa. Wengine hukonda na kuwa wembamba kama sindano kwa kukosa lishe bora

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Viwanda navyo huhitaji maji ili kuendeleza shughuli zao. Nguvu za umeme anghalabu hutolewa kwenye mianguko ya maji. Bila umeme nchi haiwezi ikastawi ipasavyo kiuchumi.

Katika nchi imani za kidini, kuna madhehebu ambayo hutumia maji kubatiza waumini wao. Watu wengi huamini ni baraka kutoka kwa mungu.

Watu wengi huuza maji na kujipatia riziki zao. Wao hutumia mitungi, mikokoteni na hata magari kusafirisha maji

Maji ni muhimu katika nyanja za usafiri . kuna maeneo makubwa ya nchi yenye maji pakee. Haya huitwa bahari abiria wanakosafiri majini hutumia meli kwa hivyo matumizi ya maji ni chungu nzima. Kwa kuwa mtaka cha mvunguni sharti ainame hatuna budi kuhifadhi maji na pia kutunza sehemu yanakotoka ili yaendelee kutufaa.

41. Kulingana na kifungu maji yameelezwa kuwa ni
    A. Hewa
    B. Mvua
    C. Uhai
    D. bahari
42. Neno ukame ni sawa na msimu upi?
    A. Kiangazi
    B. Vuli
    C. Kipupwe
    D. masika
43. Ni ukuzaji upi wa maji hutekeleza upanuzi wa uchumi wa nchi?
    A. Kupatia mifugo
    B. Kusafiria
    C. Kutolea umeme
    D. Kuoshea vyombo
44. Watu wanaosafirisha maji hawatumii
    A. Mikokoteni
    B. Mitungi
    C. Mifuko
    D. magari
45. Kulingana na kifungu kuna madhehebu ambayo _______ wao majini
    A. huwazalia
    B. huwaoza
    C. huwabatiza
    D. huwauza
46. Maneno " Chungu nzima" yametumiwa kumaanisha.
    A. Mengi
    B. Maumivu
    C. Chache
    D.
47. Kulingana na habari methali mtaka cha mvunguni sharti ainame inatutaka tufanye nini?
    A. Tutumie maji tupendavyo
    B. Tutunze vianzo vya maji
    C. Tuuze maji kwa mikokoteni
    D. Tunywe maji mengi
48. Ni nini kinachosababisha kufa na kukonda kwa wengine kulingana na habari
    A. Ukosefu wa lishe bora
    B. Lishe bora
    C. Uuzaji wa maji
    D. Unywaji wa maji
49. Kulingana na habari, yapi si matumizi ya maji?
    A. Kuosha vyombo
    B. Kuyamwaga maji
    C. Kupatia mifugo
    D. Kunyunyiza mimea
50. Kichwa kinachofaa katika kifungo hiki ni:-
    A. Umuhimu wa maji

    Chombo cha mvunguni

| | | |
|---|---|---|
| watu | B.Majiyabaharini<br>C.Uuzajiwamaji<br>D.Ubatiziwama<br>a | ji |

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM